

Maombi ya Washington Apple Health kwa Wazee, Vipofu, Walemavu/Huduma na Usaidizi wa Muda Mrefu

Tumia maombi haya kuangalia ni bima gani ya afya unayoweza kuistahiki ikiwa:

- Unahitaji Huduma na Usaidizi wa Muda Mrefu (LTSS) kama vile uuguzi wa nyumbani, kituo cha kusaidiwa kuishi, nyumba ya wazee, programu za uuguzi nyumbani, au Usaidizi Maalum kwa wazee (TSOA).
- Wewe au mtu katika kaya yako ana Medicare.
- Unahitaji msaada wa kulipia Medicare au gharama za 'coinsurance'.
- Wewe au mtu katika kaya yako ana miaka 65 au zaidi.
- Wewe au mtu katika kaya yako ana ulemavu na hana bima ya Medicare.
- Kwa TSOA: Una miaka 55 au zaidi, na wewe au mlezi wako mnahitaji usaidizi.

Kumbuka: Omba au fufua bima yako ya Apple Health mtandaoni katika Washington Healthplanfinder kupitia wahealthplanfinder.org au kwa kupiga 1-855-923-4633 ikiwa wewe ni:

- Mtu mzima mwenye miaka 19 hadi 64.
- Unaomba kwa ajili ya watoto.
- Mzazi au mlezi unayeomba kwa ajili ya watoto.
- Mjamzito au unaomba kwa ajili ya mtu ambaye ni mjamzito.

Omba kwa haraka mtandaoni

- Unaweza kuwasilisha maombi ya mtandaoni kupitia washingttonconnection.org

Taarifa zinazohitajika ili kuomba:

- Nambari ya Huduma za Kijamii
- Tarehe za kuzaliwa
- Hali ya uhamiaji
- Maelezo ya kipato
- Taarifa za rasilimali na mali (kama vile salio la akaunti za benki, hisa, hatifungani, akaunti za kustaafu)

Kwa nini tunakuomba taarifa nyingi hivyo?

- Tutatumia taarifa hizi kubaini ni bima gani ya afya unaweza kuwa na ustahiki nayo. Taarifa unayotupatia tutaitunza kwa usiri kama inavyotakiwa na sheria.

Wapi pa kutuma maombi yako yaliyojazwa na yaliyosainiwa

Kwa Apple Health ya ulemavu, bima ya Wakimbizi na bima ya wazee wenye miaka 65+, na programu zinazosaidia kulipa ada na gharama za Medicare

- Tuma maombi yako kwenda kwa:
DSHS
Community Services Division - Customer Service Center
PO Box 11699, Tacoma, WA 98411-6699
- Faksi maombi yako kwa namba 1-888-338-7410
- Peleka maombi yako kwenye Ofisi ya Huduma za Jumuiya (CSO).
- Tembelea dshs.wa.gov/esa/community-services-find-an-office kutazama maeneo
- Omba mtandaoni katika washingttonconnection.org
- Omba kwa simu kwa nambari 1-877-501-2233

Kwa huduma na usaidizi wa muda mrefu kama vile uuguzi wa nyumbani, kituo cha kusaidiwa kuishi, nyumba ya wazee, programu za uuguzi nyumbani, na TSOA.

- Tuma maombi yako kwenda kwa:

DSHS

Home and Community Services

PO Box 45826, Olympia, WA 98504-5826

- Kupata ofisi mahalia ya Huduma za Jumuiya na Nyumbani (HCS) tembelea **dshs.wa.gov/office-locations**
- Tuma maombi yako kwa faksi kupitia 1-855-635-8305
- Fanya maombi mtandaoni katika **[washingtonconnection.org](https://www.washingtonconnection.org)**
- Kwa rasilimali zaidi za LTSS tembelea **dshs.wa.gov/altsa/resources**
- Kwa rasilimali zaidi za TSOA piga 1-855-567-0252 au wasiliana na Shirika la Wazee la Eneo (AAA) la mahali ulipo ili kuzungumza na Mtaalamu wa Uangalizi wa Familia (FCS). Tafuta ofisi yako mahalia ya AAA: **[waclc.org](https://www.waclc.org)**

Haki na Wajibu wa Bima ya Afya

Haki zako (tunapaswa) kwa programu zote za bima ya afya

Kukusaidia kusoma na kujaza fomu zote zinazohitajika. Unaweza kuwasiliana na Idara ya Huduma za Afya na Jamii (DSHS) kupitia 1-877-501-2233 kwa usaidizi.

Kukupatia huduma za ukalimani na utafsiri bila gharama yoyote na bila kuchelewa wakati unapowasiliana na DSHS au Mamlaka ya Huduma ya Afya (HCA).

Kutunza faragha ya taarifa zako binafsi ila tunaweza kushirikisha baadhi ya taarifa kwa mashirika mengine ya jimbo na serikali kuu, taasisi za kifedha, na wakandarasi wa HCA kwa madhumuni ya ustahiki na uandikishaji.

Kukupa fursa ya kukata rufani usipokubaliana na ubainifu uliofanywa na DSHS au HCA ambao unaathiri ustahiki wako wa kinga ya afya, huduma na usaidizi wa muda mrefu (LTSS), au bima ya afya. Ukiomba kukata rufani, kesi yako itafanyiwa mapitio. Kwa taarifa kuhusu kukata rufani za programu za DSHS, wasiliana na Kituo cha Huduma kwa Wateja cha DSHS kupitia 1-877-501-2233 au tembelea Ofisi ya Huduma kwa Jumuiya.

Ikiwa rufani inakatwa kwa uamuzi wa bima ya Washington Apple Health, ambao haujatatuliwa kwa mapitio ya kesi, utapangiwa Usikilizaji wa Shauri la Kiutawala.

Kukutendea kwa haki. Ubaguzi ni kinyume cha sheria. DSHS na HCA zinatii sheria zinazohusika na haki za kiraia za Serikali Kuu na hazifanyi ubaguzi kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu, au jinsia. DSHS na HCA haziwatengi watu au kuwatendea tofauti kwa sababu ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu, au jinsia yao.

DSHS na HCA pia zinatii sheria husika za jimbo na hazibagui kwa misingi ya imani, udhihirisho au utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kingono, hali ya ndoa, dini, mwanajeshi aliyestaafu kwa heshima au hali ya kijeshi, au utumiaji wa mbwa mwongozi aliyepewa mafunzo au mnyama ambaye anamhudumia mtu mwenye ulemavu.

DSHS na HCA:

- Zinatoa usaidizi bila malipo na huduma kwa watu wenye ulemavu ili waweze kuwasiliana nasi kwa ufanisi, kama vile:
 - Wakalimani wa lugha ya ishara wenye sifa
 - Taarifa ya maandishi kwa muundo mwingine (herufi kubwa, sauti, miundo ya kielekroniki kwa walemavu, mifumo mingine)
- Wanatoa huduma za lugha bila malipo kwa watu ambao lugha yao ya kwanza si Kiingereza, kama vile:
 - Wakalimani wenye sifa
 - Taarifa iliyoandikwa kwa lugha nyingine

Ikiwa unahitaji huduma hizi, piga namba 1-877-501-2233.

Ukiamini kwamba DSHS au HCA zimeshindwa kutoa huduma hizi au umebaguliwa kwa namna nyingine, unaweza kuwasilisha lalamiko katika:

- **DSHS**
ATTN: Constituent Services
PO Box 45131
Olympia, WA 98504-5131
1-800-737-0617
Faksi: 1-888-338-7410
askdshs@dshs.wa.gov

- **HCA Division of Legal Services**
ATTN: Compliance Officer
PO Box 42704
Olympia, WA 98504-2704
1-855-682-0787
Faksi: 1-360-586-9551
compliance@hca.wa.gov

Unaweza kuwasilisha lalamiko wewe mwenyewe au kwa simu, barua, faksi, au barua pepe. Ukihitaji msaada kuwasilisha lalamiko, Huduma za Jimbo za DSHS au Divisheni ya Huduma za Kisheria ya HCA zinapatikana ili kukusaidia.

Unaweza pia kufungua lalamiko la haki za kiraia kielekroniki katika Idara ya Huduma za Binadamu na Afya ya Marekani, Ofisi ya Haki za Kiraia kupitia <https://ocrportal.hhs.gov/ocr/portal/lobby.jsf>, au kwa barua au simu kupitia:

U.S. Department of Health and Human Services
200 Independence Avenue SW
Room 509F, HHH Building
Washington, D.C. 20201
1-800-368-1019, 800-537-7697 (TDD).

Fomu za malalamiko zinapatikana kupitia www.hhs.gov/ocr/office/file/index.html.

Wajibu wako (unapaswa) kwa programu zote za bima ya afya

Kufichua SSN na Hali ya Uhamiaji. Isipokuwa kwa baadhi ya watu, unapaswa kutoa Nambari ya 'Social Security' (SSN) au nambari ya hati ya uhamiaji ya kwako au yeyote katika kaya yako anayetaka kuomba bima ya afya. SSN inahitajika ili kuomba fedha za kodi (tax credits) za ada za bima ya afya. Tunatumia taarifa hii kubaini ustahiki wako kwa kuthibitisha utambulisho wako, uraia wako, hali yako ya uhamiaji, tarehe ya kuzaliwa, na upatikanaji wa bima nyingine za afya. Hatushirikishi taarifa zako hizi kwa shirika lolote la uhamiaji.

Inawezekana kuomba bima kwa baadhi ya watu wa kaya yako, lakini si wengine. Ikiwa huna SSN au nambari ya hati ya uhamiaji kwa watu wote wa kaya, wengine bado wanaweza kuomba na kupata bima. Kwa mfano, unaweza kuomba kwa ajili ya mtoto wako ikiwa wewe huna ustahiki wa bima. Kuomba bima hakuwezi kuathiri hali yako ya uhamiaji au uwezekano wa kuwa mkazi wa kudumu au raia.

Pia kuna baadhi ya programu za Washington Apple Health kwa watu wasioweza kuthibitisha kuwa wapo nchini kihalali. Lakini ukiamua kutotoa SSN au nambari ya hati ya uhamiaji ya mtu mwingine katika kaya yako, tutahitaji kufanya ufuatiliaji kwako ili kupata taarifa kuhusu kipato cha mtu asiyeomba bima.

Ikiombwa na shirika, toa taarifa yoyote au ushahidi ambao unahitajika kuamua kama una ustahiki.

Mambo ya kuyafahamu kwa programu zote za bima ya afya

Kuna baadhi ya sheria za jimbo na za serikali kuu ambazo zinasimamia utendaji wa Washington Connection na mifumo ya maombi inayoedneshwa na jimbo, haki na wajibu wako kama mtu anayeitumia mifumo hiyo na kinga ya bima ambayo unaipata kwa kutumia mifumo hiyo. Kwa kutumia mifumo hii, unakubali kutii sheria zinazohusika kwa mtu anayetumia mifumo hiyo na kinga ya bima anayopata kutokana na kutumia mifumo hiyo.

Sheria ya Taifa ya Usajili wa Mpiga Kura ya 1973 inahitaji majimbo yote kutoa usaidizi wa usajili wa mpiga kura kupitia ofisi zao za msaada kwa umma. Kuomba kujiandikisha au kukataa kujiandikisha kupiga kura hakutaathiri huduma au mafao ambayo utapatwa na shirika hili. Jiandikishe kupiga kura hapa www.vote.wa.gov au omba fomu za kuandikisha mpiga kura 1-800-448-4881.

Vikwazo vya Sheria ya Uhamishaji na Uwajibikaji wa Bima ya Afya (HIPAA) vinazuia HCA na DSHS kujadili taarifa ya kiafya ya kwako au mtu yeyote wa kaya yako na mtu yeyote, ikiwemo mwakilishi aliyeidhinishwa, isipokuwa tu kama mtu huyo awe na mamlaka ya uwakilishi (power of attorney) au iwapo wewe umesaini fomu ya ridhaa ukiidhinisha ufichuzi wa taarifa hii. Hii inajumuisha ufichuzi wa taarifa ya afya ya akili, WVU, UKIMWI, majibu ya vipimo vya Magonjwa ya Zinaa, au matibabu na huduma za utegemezi wa kemikali.

Sheria ya Matibabu Nafuu (ACA) inaizuia DSHS na HCA kutoa taarifa zenye utambulisho binafsi (PII) za kwako au mtu yeyote wa kaya yako kwa mtu yeyote ambaye hajaidhinishwa kuzipokea, na bila ridhaa yako.

Taarifa ambayo unaipa DSHS na HCA itafanyiwa uthibitisho na maafisa wa serikali kuu na wa jimbo kwa madhumuni ya kubaini ustahiki wako wa kinga ya bima ya afya. Uthibitishaji unaweza kujumuisha kuendesha ufuatiliaji wa wahusika utakaofanywa na wafanyakazi wa shirika.

HCA na DSHS haziwajibiki kwa usimamiaji wa bima yako ya afya. Kampuni yako ya bima ya afya inaweza kukupa taarifa zaidi kuhusu mafao yako. **Ukiwa na maswali kuhusu vigezo vya bima yako ya afya, ikiwemo mafao yapi una ustahiki nayo, na kudai mafao au kukata rufani ya kukataliwa mafao, unapaswa kuwasiliana na kampuni yako ya bima ya afya.**

Unaweza kuomba huduma za kushurutisha matunzo kupitia Divisheni ya Matunzo ya Watoto (DCS).

Kupata maombi ya huduma hizi, tembelea www.childsupportonline.wa.gov au wasiliana na ofisi yako mahalia ya DCS.

Haki zako (tunapaswa) kwa Washington Apple Health tu

Kukuelezea haki na wajibu wako ikiwa utaomba hivyo.

Kukuruhusu kutuma sehemu ya maombi inayojumuisha angalau, jina lako, anwani, saina yako au saina ya mwakilishi aliyeidhinishwa wa mwombaji. Siku tunayopata sehemu ya maombi ndyo tarehe ya maombi yako, ambayo inaweza kuathiri lini bima yako itatmika rasmi. Hatutatoa uamuzi wa mwisho kuhusu bima yako hadi baada ya kuwa umekamilisha maombi yako.

Kukuruhusu kuwasilisha maombi au sehemu ya maombi yako kwa kutumia njia iliyoainishwa chini ya WAC 182-503-0005.

Kushughulikia maombi yako haraka na si baadaye zaidi ya muda ulioainishwa katika WAC 182-503-0060.

Kukupa siku 10 za kalenda kutupatia taarifa tunazohitaji ili kubaini ustahiki. Ukiomba muda zaidi, tutakupa muda zaidi. Usipotupatia taarifa au usipoomba muda zaidi, tunaweza kukunyima, kuifunga, au kuibadili bima yako ya afya.

Kukusaidia ukipata changamoto kupata taarifa yoyote au ushahidi unaohitajika kwetu ili kuamua kama una ustahiki. Kama tutahitaji nyaraka ambayo inagharimu fedha, tutaiomba na tutalipa gharama.

Kukutaarifu, kadri iwezekanavyo, angalau siku 10 kabla ya kusitisha kinga ya bima yako ya afya.

Kukupa maamuzi ya maandishi, kwenye kesi nyingi, ndani ya siku 45. Kinga ya Bima ya afya kwa baadhi ya kesi za ulemavu inaweza kuchukua hadi siku 60. Tunatoa uamuzi wa maandishi kwa matibabu ya ujauzito ndani ya siku 15.

Kukuruhusu kukataa kuzungumza na mchunguzi ikiwa tunafanya ukaguzi wa kesi yako. Hulazimiki kumruhusu mchunguzi aingie nyumbani kwako. Unaweza kumwomba mchunguzi aje wakati mwingine. Ombi kama hilo halitaathiri ustahiki wako wa kinga ya bima ya afya.

Kuendelea na kinga ya bima ya Washington Apple Health wakati tukiamua iwapo una ustahiki wa programu nyingine kwa mujibu wa WAC 182-504-0125.

Kukupa huduma za haki sawa za ufikio kama ilivyoielezwa katika WAC 182-503-0120 ikiwa una ustahiki.

Wajibu wako (unapaswa) kwa Washington Apple Health tu

Kuripoti mabadiliko kama inavyotakiwa katika WAC 182-504-0105 and WAC 182-504-0110 ndani ya siku 30 za badiliko. Kusoma barua yako ya idhinisho ili kuona ni mabadiliko gani unapaswa kuyaripoti.

Kufufua bima ukiombwa kufanya hivyo.

Kutoa taarifa za watoa huduma ya kitiba inayohitajika kututoza sisi kwa ajili ya huduma za afya.

Kuomba Medicare ikiwa una haki ya kuwa nayo.

Kutoa ushirikiano kwa watu wa Uhakikisho wa Ubora.

Kuomba na kufanya jitihada ya kutosha kupata kipato kutoka vyanzo vingine wakati unaomba au kupokea kinga ya bima ya Washington Apple Health.

Mambo ya kuyafahamu kwa Washington Apple Health tu

Kwa kuomba na kupokea Washington Apple Health, unalipa jimbo la Washington haki zote za usaidizi wowote wa kitiba na za malipo ya wahusika wa tatu wa huduma ya afya.

Shirika linaweza kushirikisha historia ya chanjo ya mtoto wako kwa Mfumo wa Kufuatilia Chanjo za Watoto (CPITS).

Taarifa unayoripoti inaweza kushirikishwa kwa DSHS ili kubaini ustahiki na mafao ya kila mwezi kwa programu kama vile kinga ya bima ya afya, usaidizi wa pesa taslimu, usaidizi wa chakula na ruzuku za ulezi wa watoto.

Kisheria, Jimbo la Washington linaweza kurejesha gharama ilizolipa kwa huduma za aina fulani za kitiba kutoka kwenye mali yako ya urithi kupitia ‘Estate Recovery’ (RCW 41.05A.090, RCW 43.20B.080, na Chapter 182-527 WAC). ‘Estate Recovery’ haifanyiki hadi baada ya kifo chako, kifo cha mwenzi wako aliyesalia, na watoto wako waliosalia wawe na miaka 21 au zaidi. Pia haifanyiki ikiwa mtoto aliyesalia alikuwa kipofu/mlemavu wakati wa kifo chako. Gharama zinazopaswa kurejeshwa zinajumuisha:

- Baadhi ya huduma na usaidizi wa muda mrefu wa Washington Apple Health, ikiwa ulikuwa na miaka 55 au zaidi wakati ulipopokea huduma;
- Baadhi ya huduma zinazofadhiliwa na jimbo tu, bila kujali umri wako wakati ulipopokea huduma.

Unaweza kupata orodha ya huduma zinazopaswa kurejeshwa gharama kwenye WAC 182-527-2742. Unaweza kupata orodha ya mali zisizohusika katika urejeshaji kwa mujibu wa WAC 182-527-2746.

Jimbo linaweza pia kufaili umiliki kabla ya kifo wa nyumba yako, katika umri wowote, ikiwa utawekwa kwenye taasisi kwa kipindi cha maisha yako yote (WAC 182-527-2734). Jimbo linaweza kurejesha gharama baada ya mauzo ya nyumba, au mali yako ya urithi, isipokuwa:

- Mwenzi wako anaishi katika nyumba hiyo;
- Ndugu yako anaishi katika nyumba hiyo, ni mmiliki mwenza, na anakidhi baadhi ya vigezo.
- Mtoto wako anaishi katika nyumba hiyo, na ni kipofu/mlemavu; au
- Mtoto wako anaishi katika nyumba hiyo na ana chini ya miaka 21.

Pata orodha ya huduma zinazopaswa kurejeshwa gharama chini ya umiliki kabla ya kifo katika WAC 182-527-2734.

Unaweza kuwekewa ukomo wa mtoa huduma mmoja, duka moja la dawa, na/au hospitali moja ikiwa utaomba huduma za afya zisizo za lazima kutoka kwa watoa huduma.

[English] Language assistance services, including interpreters and translation of printed materials, are available free of charge. Call 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Amharic] የቋንቋ እገዛ አገልግሎት፣ አስተርጓሚ እና የሰነዶችን ትርጉም ጨምሮ በነጻ ይገኛል። 1-800-562-3022 (TRS: 711) ይደውሉ።

[Arabic] خدمات المساعدة في اللغات، بما في ذلك المترجمين الفوريين وترجمة المواد المطبوعة، متوفرة مجاناً، اتصل على رقم 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Burmese] ဘာသာပြန်ဆိုသူများနှင့် ထုတ်ပြန်ထားသည့် စာရွက်စာတမ်းများဘာသာပြန်ခြင်းအပါအဝင် ဘာသာစကားအထောက်အကူဆောင်ရွက်မှုများကို အခမဲ့ရရှိနိုင်ပါသည်။ 1-800-562-3022 (TRS: 711) ကိုဖုန်းခေါ်ဆိုပါ။

[Cambodian] សេវាជំនួយភាសា រួមមានទាំងអ្នកបកប្រែផ្ទាល់មាត់ និង ការបកប្រែឯកសារបោះពុម្ព គឺអាចរកបានដោយឥតគិតថ្លៃ។ ហៅទូរស័ព្ទទេវលេខ 1-800-562-3022 (TRS: 711)។

[Chinese] 免费提供语言协助服务，包括口译员和印制资料翻译。请致电 1-800-562-3022 (TRS: 711)。

[Korean] 통역 서비스와 인쇄 자료 번역을 포함한 언어 지원 서비스를 무료로 이용하실 수 있습니다. 1-800-562-3022 (TRS: 711)번으로 전화하십시오.

[Laotian] ການບໍລິການດ້ານພາສາ, ລວມທັງນາຍແປພາສາ ແລະ ການແປເອກສານຕີພິມ, ມີໄວ້ໃຫ້ພຣິໄດຍບໍ່ຄິດຄ່າ. ໂທຫາເລກ 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Oromo] Tajajilli gargaarsa afaanii, nama afaan hiikuu fi ragaalee maxxanfaman hiikuun, kaffaltii malee ni argattu. 1-800-562-3022 (TRS: 711) irratti bilbilaa.

[Persian] خدمات کمک زبانی، از جمله مترجم شفاهی و ترجمه اسناد و مدارک (مطالب) چاپی، بصورت رایگان ارائه خواهد شد. یا شماره 1-800-562-3022 تماس بگیرید. (TRS: 711)

[Punjabi] ਭਾਸ਼ਾ ਸਹਾਇਤਾ ਸੇਵਾਵਾਂ—ਦੁਭਾਸ਼ੀਏ ਅਤੇ ਪ੍ਰਿੰਟ ਕੀਤੀ ਹੋਈ ਸਮੱਗਰੀ ਦੇ ਅੰਨੁਵਾਦ ਸਮੇਤ—ਮੁਫਤ ਉਪਲੱਬਧ ਹਨ। 1-800-562-3022 (TRS: 711) 'ਤੇ ਕਾਲ ਕਰੋ।

[Romanian] Serviciile de asistență lingvistică, inclusiv cele de interpretariat și de traducere a materialelor imprimate, sunt disponibile gratuit. Apelați 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Russian] Языковая поддержка, в том числе услуги переводчиков и перевод печатных материалов, доступна бесплатно. Позвоните по номеру 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Somali] Adeego caawimaad luuqada ah, ay ku jirto turjubaano afka ah iyo turjumid lagu sameeyo waraaqaha la daabaco, ayaa lagu helayaa lacag la'aan. Wac 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Spanish] Hay servicios de asistencia con idiomas, incluyendo intérpretes y traducción de materiales impresos, disponibles sin costo. Llame al 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Swahili] Huduma za msaada wa lugha, ikiwa ni pamoja na wakalimani na tafsiri ya nyaraka zilizochapishwa, zinapatikana bure bila ya malipo. Piga 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Tagalog] Mga serbisyong tulong sa wika, kabilang ang mga tagapagsalin at pagsasalin ng nakalimbag na mga kagamitan, ay magagamit ng walang bayad. Tumawag sa 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Tigrigna] ተርጉምትን ናይ ዝተፀሓፉ ማተርያላት ትርጉምን ሓዊሱ ናይ ቋንቋ ሓገዝ ግልጋሎት፤ ብዘይ ምንም ክፍሊት ይርከቡ። ብ 1-800-562-3022 (TRS: 711) ደውል።

[Ukrainian] Мовна підтримка, у тому числі послуги перекладачів та переклад друкованих матеріалів, доступна безкоштовно. Зателефонуйте за номером 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Vietnamese] Các dịch vụ trợ giúp ngôn ngữ, bao gồm thông dịch viên và bản dịch tài liệu in, hiện có miễn phí. Gọi 1-800-562-3022 (TRS: 711).

Maombi ya Washington Apple Health kwa Wazee, Vipofu, Walemavu/ Huduma na Usaidizi wa Muda Mrefu

1

Jina la mwombaji na taarifa ya mawasiliano

Jina la kwanza (Mwenyewe)

La kati

Jina la mwisho

Nambari ya ID ya Mteja (Kama inahusika)

Saini ya mwombaji au mwakilishi aliyeidhinishwa

Anwani ya mahali unapoishi (Inatakiwad)

Wilaya

Mji

Jimbo

Msimbo wa posta

Tiki kisanduku hiki ikiwa huna anwani ya makazi

Anwani ya barua (ikiwa ni tofauti)

Wilaya

Mji

Jimbo

Msimbo wa posta

Nambari ya simu ya msingi

Simu ya mkononi

Barua pepe

Ikiwa unaishi kwenye kituo, andika jina la kituo na anwani, kama haifanani na ya hapo juu:

Jina la kituo

Anwani ya kituo

Wilaya

Mji

Jimbo

Msimbo wa posta



18005

2**Programu inayoombwa**

Mimi, mwenzi wangu, au mtu katika kaya yangu anaomba:

Huduma za Mlezi wa Nyumbani

Bima ya Afya kwa Wazee, Vipofu, au Walemavu

Usaidizi wa Kuishi/Nyumba ya Familia ya Wazee

Programu ya Punguzo la Medicare

Uuguzi wa Nyumbani

Apple Health kwa Wafanyakazi Walemavu (HWD)

Usaidizi Maalum kwa Wazee (TSOA)

3**Taarifa za bili ya matibabu ambayo haijalipwa**

Je, wewe au mtu yeyote unayemuomba mnahitaji msaada wa kulipia bili za matibabu ambazo hazijalipwa zilizotozwa katika miezi yoyote 3 kabla ya mwezi wa sasa? Ndio Hapana Ikiwa ndio, ainisha nani:

4**Taarifa za lugha**

Je, wewe au yeyote unayemuomba mnahitaji mkalimani au kupokea nyaraka kwa lugha nyingine?

Ndio Hapana

Ikiwa ndio, mnahitaji lugha gani au muundo gani mbadala? Orodhesha zote zinazohusika: _____

5**Taarifa kuhusu wewe na familia yako**

Jiandike wewe mwenyewe, mwenzi, na tegemezi wanaoishi nawe hata kama huwaombe (ikiwezekana ambatisha karatasi za ziada).

		MWENYEWE	
_____	_____	_____	_____
Jina (La kwanza, Kati, Mwisho)	Jinsia ya kuzaliwa	Uhusiano na wewe	Tarehe ya kuzaliwa

_____	_____	_____	_____
Nambari ya Ruzuku ya Serikali (SSN)*	Je, unataka bima kwa ajili ya mtu huyu?	Ndio	Hapana

Raia au Si Raia: (tiki moja)

Raia wa Marekani	Ndio	Hapana	Mkazi wa Washington	Ndio	Hapana
------------------	------	--------	---------------------	------	--------

Je, una asili ya Kihispania, Kilatini, au Kihispania? (HIARI)

Mkyuba	Mmeksiko/Mmarekani	Mmeksiko/Mchikano	Sio Mhispania
Mhispania/Asili ya Kihispania Nyengine	Mpwetorika		

Mbari (HIARI – chagua hadi tano zinazohusika)

Muhindi Mwamerika au Mzawa wa Alaska	Mchina	Mkorea	Mtai
Mwasia	Mfilipino	Mlaotia	Mvetinamu
Mhindi Mwasia	Mguamania	Mwanakisiwa cha Pasifiki Kingine	Mweupe

Mweusi au Mmarekani Mwafrika	Mhawai	Mbari Nyingine
Mkambodia	Mjapani	Msamoa

Jina (La kwanza, Kati, Mwisho)	Jinsia ya kuzaliwa	Uhusiano na wewe?	Tarehe ya kuzaliwa
--------------------------------	--------------------	-------------------	--------------------

Nambari ya Ruzuku ya Serikali (SSN)*	Je, unataka bima kwa ajili ya mtu huyu?	Ndio	Hapana
--------------------------------------	---	------	--------

Raia au Si Raia: (tiki moja)

Raia wa Marekani	Ndio	Hapana	Mkazi wa Washington	Ndio	Hapana
------------------	------	--------	---------------------	------	--------

Je, una asili ya Kihispania, Kilatini, au Kihispania? (HIARI)

Mkyuba	Mmeksiko/Mmarekani Mmeksiko/Mchikano	Sio Mhispania
Mhispania/Asili ya Kihispania Nyengine	Mpwetorika	

Mbari (HIARI – chagua hadi tano zinazohusika)

Muhindi Mwamerika au Mzawa wa Alaska	Mchina	Mkorea	Mtai
Mwasia	Mfilipino	Mlaotia	Mvetinamu
Mhindi Mwasia	Mguamania	Mwanakisiwa cha Pasifiki Kingine	Mweupe
Mweusi au Mmarekani Mwafrika	Mhawai	Mbari Nyingine	
Mkambodia	Mjapani	Msamoa	

Jina (La kwanza, Kati, Mwisho)	Jinsia ya kuzaliwa	Uhusiano na wewe?	Tarehe ya kuzaliwa
--------------------------------	--------------------	-------------------	--------------------

Nambari ya Ruzuku ya Serikali (SSN)*	Je, unataka bima kwa ajili ya mtu huyu?	Ndio	Hapana
--------------------------------------	---	------	--------

Raia au Si Raia: (tiki moja)

Raia wa Marekani	Ndio	Hapana	Mkazi wa Washington	Ndio	Hapana
------------------	------	--------	---------------------	------	--------

Je, una asili ya Kihispania, Kilatini, au Kihispania? (HIARI)

Mkyuba	Mmeksiko/Mmarekani Mmeksiko/Mchikano	Sio Mhispania
Mhispania/Asili ya Kihispania Nyengine	Mpwetorika	

Mbari (HIARI – chagua hadi tano zinazohusika)

Muhindi Mwamerika au Mzawa wa Alaska	Mchina	Mkorea	Mtai
Mwasia	Mfilipino	Mlaotia	Mvetinamu
Mhindi Mwasia	Mguamania	Mwanakisiwa cha Pasifiki Kingine	Mweupe
Mweusi au Mmarekani Mwafrika	Mhawai	Mbari Nyingine	
Mkambodia	Mjapani	Msamoa	

_____ Jina (La kwanza, Kati, Mwisho) _____ Jinsia ya kuzaliwa _____ Uhusiano na wewe? _____ Tarehe ya kuzaliwa

_____ Nambari ya Ruzuku ya Serikali (SSN)* _____ Je, unataka bima kwa ajili ya mtu huyu? _____ Ndio _____ Hapana

Raia au Si Raia: **(tiki moja)**

Raia wa Marekani _____ Ndio _____ Hapana _____ Mkazi wa Washington _____ Ndio _____ Hapana

Je, una asili ya Kihispania, Kilatini, au Kihispania? (HIARI)

Mkyuba _____ Mmeksiko/Mmarekani Mmeksiko/Mchikano _____ Sio Mhispania

Mhispania/Asili ya Kihispania Nyengine _____ Mpwetorika

Mbari (HIARI – chagua hadi tano zinazohusika)

Muhindi Mwamerika au Mzawa wa Alaska	Mchina	Mkorea	Mtai
Mwasia	Mfilipino	Mlaotia	Mvetinamu
Mhindi Mwasia	Mguamania	Mwanakisiwa cha Pasifiki Kingine	Mweupe
Mweusi au Mmarekani Mwafrika	Mhawai	Mbari Nyingine	
Mkambodia	Mjapani	Msamoa	

_____ Jina (La kwanza, Kati, Mwisho) _____ Jinsia ya kuzaliwa _____ Uhusiano na wewe? _____ Tarehe ya kuzaliwa

_____ Nambari ya Ruzuku ya Serikali (SSN)* _____ Je, unataka bima kwa ajili ya mtu huyu? _____ Ndio _____ Hapan

Raia au Si Raia: **(tiki moja)**

Raia wa Marekani _____ Ndio _____ Hapana _____ Mkazi wa Washington _____ Ndio _____ Hapana

Je, una asili ya Kihispania, Kilatini, au Kihispania? (HIARI)

Mkyuba _____ Mmeksiko/Mmarekani Mmeksiko/Mchikano _____ Sio Mhispania

Mhispania/Asili ya Kihispania Nyengine _____ Mpwetorika

Mbari (HIARI – chagua hadi tano zinazohusika)

Muhindi Mwamerika au Mzawa wa Alaska	Mchina	Mkorea	Mtai
Mwasia	Mfilipino	Mlaotia	Mvetinamu
Mhindi Mwasia	Mguamania	Mwanakisiwa cha Pasifiki Kingine	Mweupe
Mweusi au Mmarekani Mwafrika	Mhawai	Mbari Nyingine	
Mkambodia	Mjapani	Msamoa	

*HCA haishirikishi taarifa hii kwa shirika lolote la uhamiaji kwa madhumuni ya ushurutishaji wa masuala ya uhamiaji. Acha hapa wazi kama huna SSN.

6

Taarifa za Jumla

1. Katika siku 30 zilizopita, mimi, mwenzi wangu, au mtu katika kaya yangu alipata bima ya afya kutoka jimbo lingine, kabila lingine au chanzo kingine?

Ndio Hapana Ikiwa ndio, eleza _____

2. Mimi, mwenzi wangu, au mtu katika kaya yangu alipata Kipato cha Ulinzi wa Ziada (SSI) katika jimbo lingine?

Ndio Hapana Ikiwa ndio, nani? _____

3. Mimi, na mwenzi wangu, au mtu mwengine katika kaya yangu ni mhamiaji aliyedhaminiwa?

Ndio Hapana Ikiwa ndio, nani? _____

4. Mimi, mwenzi wangu, au mtu katika kaya yangu ametumikia katika Jeshi la Marekani, Mgambo, au Jeshi la Akiba au amekuwa tegemezi au mwenzi wa mtu aliyetumikia majeshi:

Ndio Hapana Ikiwa ndio, nani? _____

5. Nina tegemezi wa kodi ambaye bado sijamjumuisha kwenye maombi yangu ambaye haishi na mimi?

Ndio Hapana Ikiwa ndio, Orodhesha majina ya tegemezi wa kodi _____

6. Mimi ni: Mseja Nina ndoa na naishi na mwenzi Nina ndoa na siishi na mwenzi Mtalaka Mjane

Naishi Kinyumba Nimetengana kihalali

7

Kipato cha ajira au kujijiri (Ambatisha ushahidi)

Kipato ni pesa inayotengenezwa kutokana na ajira au kujijiri, baadhi ya mifano* inajumuisha

Ajira:

- Ujira, mshahara au bakshishi ambayo inawekewa zuio na kodi za mapato za serikali kuu kwenye Fomu W-2, boksi 1
- Marupurupu na kamisheni.
- Malipo ya pensheni.
- Kipato kutokana na kazi ambayo mwajiri wako hakuzuia kodi (kama vile kazi za mtandaoni)

- Kuendesha gari la ukodishaji wa safari au uwasilishaji wa bidhaa
- Kufanya kazi za kutumwa au kufanya kazi ndogondogo
- Kuuza bidhaa mtandaoni
- Kutoa huduma za kibunifu au kitaalamu
- Kufanya kazi nyingine za muda, kadri ya uhitaji au za kujitegemea
- Mafao kutokana na mgomo wa chama cha ushirika

Ajira Binafsi:

- Kumiliki au kuendesha biashara
- Kumiliki au kuendesha shamba
- Mtumishi au mjumbe wa taasisi ya kidini
- Mwajiriwa asiyezuiwa kodi (statutory employee) na ana kipato

***Chanzo: irs.gov/credits-deductions/individuals/earned-income-tax-credit/earned-income-and-earned-income-tax-credit-eitc-tables**

1. Mimi, mwenzi wangu, au mtu nayemuomba ana kipato kinachotokana na kazi Ndio Hapana Ikiwa ndio, tafadhali jaza sehemu hii.

2. _____ Nani analipwa kipato hiki _____ Jina la mwajiri _____ Nambari ya simu ya mwajiri _____

_____ Je, kazi hii ni ajira binafsi? Ndio Hapana

Tarehe ya kuanza _____

Kiwango cha jumla kilichopokewa (kiwango cha dola kabla ya makato) _____ kila baada ya: Saa Wiki Wiki mbili

Mara mbili kwa mwezi Mwezi

_____ Masaa kwa wiki

_____ Tarehe za malipo (kwa mfano., 1st na 15th, au kila Ijumaa)

3. _____ Nani analipwa kipato hiki: _____ Jina la mwajiri _____ Simu ya mwajiri _____

_____ Je, kazi hii ni ajira binafsi? Ndio Hapana

Tarehe ya kuanza _____

GKiwango cha jumla kilichopokewa (kiwango cha dola kabla ya makato) _____ kila baada ya: Saa Wiki Wiki mbili

Mara mbili kwa mwezi Mwezi

8

Kipato Kingine (Kwa watu wote wa kaya) (Ambatisha ushahidi)

1. Mifano ya kipato kingine ni:

- Msaada wa Mtoto au Kumkimu Mwenzi
- Mafao ya elimu (Mikopo ya Wana-funzi, Misaada, Masomo-Kazi)
- Kipato cha Michezo
- Zawadi (Usaidizi wa Pesa Taslimu/ Kadi za Zawadi)
- Riba/Gawio
- Kazi na Viwanda (L&I)
- Mafao ya njia ya Reli
- Kipato cha upangaji
- Kiinua mgongo cha kustaafu
- Mikataba ya Mauzo/Hati za Made-ni (Promissory Notes)
- Usalama wa Jamii
- Kipato cha Nyongeza cha Usalama (SSI)
- Kipato cha kabila
- Amana
- Mafao ya Kutoajiriwa
- Mafao ya Utawala wa Askari wastaafu (VA) au Jeshi
- Mingine

2. Orodhesha kipato kingine ambacho wewe, mwenzi wako, au yeyote unayemuomba anakipokea:

_____ Aina nyingine ya kipato _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla

_____ Aina nyingine ya kipato _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla

_____ Aina nyingine ya kipato _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla

_____ Aina nyingine ya kipato _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla

_____ Aina nyingine ya kipato _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla _____ Nani anapata kipato hicho _____ Kiasi cha mwezi cha jumla

3. Mimi, mwenzi wangu, au mtu katika kaya yangu anapata kipato kinachotokana na uwekezaji wa 'annuity'?

Ndio Hapana

_____ Nani anamiliki annuity hio _____ Kampuni au taasisi _____ Kiasi au thamani _____ Kipato cha mwezi _____ Tarehe ya kununua

_____ Nani anamiliki annuity hio _____ Kampuni au taasisi _____ Kiasi au thamani _____ Kipato cha mwezi _____ Tarehe ya kununua

9

Gharama za Nyumba (Ambatisha ushahidi ikiwa unaomba LTSS)

_____ Kodi _____ Mkopo wa nyumba _____ Mkopo wa sehemu _____ Bima ya wamiliki nyumba _____ Kodi za majengo _____ Gharama nyingine

Je, unapokea msaada kutoka kwa mtu au shirika lingine, kama vile makazi nafuu, ambalo linalipia gharama hizi au sehemu?

Ndio Hapana Ikiwa ndio, nani? _____

10

Makato

1. Mimi, mwenzi wangu, au mtu nayemuomba malipo au anayepaswa kulipa:

_____ Ulezi wa mtoto au mtu mzima tegemezi _____ Kiwango cha kila mwezi _____ Nani analipa

_____ Matunzo ya watoto yaliyoamriwa na mahakama _____ Kiwango cha kila mwezi _____ Nani analipa

_____ Ada za mlipwaji _____ Kiwango cha kila mwezi _____ Nani analipa

_____ Ada za ulezi _____ Kiwango cha kila mwezi _____ Nani analipa

_____ Ada za mwanasheria zilizoamriwa na mahakama _____ Kiwango cha kila mwezi _____ Nani analipa

_____ Gharama za matibabu za mara kwa mara _____ Kiwango cha kila mwezi _____ Nani analipa
(jumuisha Medicare au ada nyingine za bima ya afya unazolipa)

2. Mimi, mwenzi wangu, au mtu nayemuomba anadaiwa gharama za matibabu?

_____ Aina ya gharama ya matibabu _____ Tarehe ya kutozwa _____ Kiasi Kinachodaiwa _____ Nani anadaiwa

_____ Aina ya gharama ya matibabu _____ Tarehe ya kutozwa _____ Kiasi Kinachodaiwa _____ Nani anadaiwa

_____ Aina ya gharama ya matibabu _____ Tarehe ya kutozwa _____ Kiasi Kinachodaiwa _____ Nani anadaiwa

3. Mimi, mwenzi wangu, au mtu nayemuomba ana ulemavu na anafanya kazi na ana gharama zinazotegemeza ajira? Hizi zinaitwa Gharama za Kazi Zinazohusiana na Ulemavu (IRWE):

Ndio Hapana Ikiwa ndio, Andika kiasi cha IRWE _____

11

Mali (Ambatisha Ushahidi)

(Ruka sehemu hii ikiwa unaomba tu Programu za Punguzo la Medicare (MSP) au Apple Health Kwa Wafanyakazi Walemavu (HWD))

1. Chanzo ni kitu chochote ambacho unamiliki au kununua ambacho kinaweza kuuzwa, kufanyia biashara, au kubadilisha kwa fedha taslimu au fedha zilizozuliwa na wengine. Mali hapa haijumuishi mali binafsi kama vile samani, bidhaa za ndani ya nyumba, au mavazi. Mifano ya vyanzo ni:

- Fedha taslimu
- Akaunti za cheki
- Akaunti za akiba
- CDs
- Akaunti ya fedha za masoko
- Hatifungani za kuweka akiba (savings bonds)
- Bondi
- Mifuko ya uwekezaji wa pamoja (mutual funds)
- Hisa (stocks)
- Malipo ya kila mwaka (annuities)
- Amana
- IRA
- 401K
- Mfuko wa kustaafu
- Nyumba, ikiwemo unayoi-shi kwa sasa
- Fedha za maziko (burial funds)
- Jengo la makazi (condominium)
- Ardhi
- Mkataba wa mauzo (sales contract)
- Majengo
- Nyumba ya maisha (Life estate)
- Bima ya Maisha
- Maziko yaliyolipiwa kabla (pre-paid funeral)
- Mfuko wa chuo
- Majengo ya mapumziko ya likizo (time-share)
- Vifaa vya biashara
- Vifaa vya shambani
- Mifugo

2. Orodhesha vyanzo ambavyo wewe, na mwenzi wako, au mtu unaemuomba anamiliki au kununua:

_____	_____	_____	_____	_____	_____	_____
Aina ya rasilimali	Nani anamiliki	Eneo	Thamani	Nani anamiliki	Eneo	Thamani
_____	_____	_____	_____	_____	_____	_____
Aina ya rasilimali	Nani anamiliki	Eneo	Thamani	Nani anamiliki	Eneo	Thamani
_____	_____	_____	_____	_____	_____	_____
Aina ya rasilimali	Nani anamiliki	Eneo	Thamani	Nani anamiliki	Eneo	Thamani
_____	_____	_____	_____	_____	_____	_____
Aina ya rasilimali	Nani anamiliki	Eneo	Thamani	Nani anamiliki	Eneo	Thamani

3. Mimi, mwenzi wangu, au mtu nayemuomba ana magari, malori, gari za kati, mashua, RV, matrela, au motokaa nyingine:

_____	_____	_____	_____
Mwaka (mfano, 2010)	Kutengenezwa (mfano, Ford)	Aina (mfano, Escort)	Kiasi kinachodaiwa
_____	_____	_____	_____
Tiki kama imekodishwa	Tiki kama inatumika kwa madhumuni ya matibabu		
_____	_____	_____	_____
Mwaka (mfano, 2010)	Kutengenezwa (mfano, Ford)	Aina (mfano, Escort)	Kiasi kinachodaiwa
_____	_____	_____	_____
Tia tiki ikiwa ni ya kukodisha	Tiki kama inatumika kwa madhumuni ya matibabu		

12

Mali za Ziada za LTSS (Jaza tu ikiwa unatuma maombi ya huduma za LTSS)

1. Mimi, mwenzi wangu, au mtu nayemuomba anamiliki au ananunua nyumba ambayo ni makazi makuu:

_____	_____	_____
Anwani ya nyumba	Thamani ya sasa (Kulingana na mtathmini)	Kiasi cha mkopo kinachodaiwa kwenye nyumba
_____	_____	_____
Anwani ya nyumba	Thamani ya sasa (Kulingana na mtathmini)	Kiasi cha mkopo kinachodaiwa kwenye nyumba

2. Mimi, mwenzi wangu, au mtu nayemuombea ameza, amebadilishana, ametoa, au amehamisha mali katika miaka mitano iliyopita (ikiwemo mifuko ya makazi, magari, pesa taslimu, au nyumba ya maisha)? Ndio Hapana Ikiwa ndio, jaza taarifa zifuatazo: (ikihitajika ambatisha karatasi za ziada)

13 **Bima ya Afya ya Muda Mrefu (Haihitajiki kwa Programu za Punguzo la Medicare)**

Mimi/sisi tuna bima ya afya ya muda mrefu? Ndio Hapana Hii ni sera yenye ustahiki ya Ubia wa LTC (LTCP)?

Ndio Hapana

Ikiwa ndio, tafadhali orodhesha jina la kampuni ya bima na nani anayekingwa na sera:

Kuongeza maelezo yoyote ya ziada kwenye maombi haya, ambatisha karatasi yenye taarifa husika.

14 **Taarifa ya Mwakilishi Aliyeidhinishwa**

Mwakilishi aliyeidhinishwa ni mtu mzima yeyote anayetambua mazingira ya kaya na ameidhinishwa na kaya kutenda kwa niaba ya kaya kwa madhumuni ya ustahiki.

Kwa kumteua mwakilishi aliyeidhinishwa, unatoa ruhusa kwa mwakilishi wako aliyeidhinishwa:

- Kusaini maombi kwa niaba yako;
- Kupokea notisi zinazohusiana na maombi na akaunti yako; na
- Kutenda kwa niaba yako kwenye masuala yote yanayohusiana na maombi na akaunti.

1. Je, unamteua mwakilishi aliyeidhinishwa? Ndio Hapana

2. Je, unataka mwakilishi wako aliyeidhinishwa kupokea notisi zinazohusiana na maombi na akaunti yako?

Ndio Hapana

3. Je, mwakilishi huyu aliyeidhinishwa ni mlezi halali kisheria

Ndio Hapana Ikiwa ndio, kwa nani: _____

4. Je, mwakilishi huyu aliyeidhinishwa ana mamlaka ya uwakilishi?

Ndio Hapana Ikiwa ndio, kwa nani: _____

Kuilipa Jimbo kwa ajili ya Kinga ya Bima ya Afya na Matibabu ya Muda Mrefu:

Kisheria, Jimbo la Washington linaweza kurejesha gharama ilizolipa kwa huduma za aina fulani za kitiba kutoka kwenye mali yako ya urithi kupitia 'Estate Recovery' (RCW 41.05A.090, RCW 43.20B.080, na Chapter 182-527 WAC). 'Estate Recovery' haifanyiki hadi baada ya kifo chako, kifo cha mwenzi wako aliyesalia, na watoto wako waliosalia wawe na miaka 21 au zaidi. Pia haifanyiki ikiwa mtoto aliyesalia alikuwa kipofu/mlemavu wakati wa kifo chako. Gharama zinazopaswa kurejeshwa zinajumuisha:

Baadhi ya huduma na usaidizi wa muda mrefu wa Washington Apple Health, ikiwa ulikuwa na miaka 55 au zaidi wakati ulipopokea huduma.

Baadhi ya huduma zinazofadhiliwa na jimbo tu, bila kujali umri wako wakati ulipopokea huduma.

Unaweza kupata orodha ya huduma zinazopaswa kurejeshwa gharama kwenye WAC 182-527-2742. Unaweza kupata orodha ya mali zisizohusika katika urejeshaji kwa mujibu wa WAC 182-527-2746.

Jimbo linaweza pia kufaili umiliki kabla ya kifo wa nyumba yako, katika umri wowote, ikiwa utawekwa kwenye taasisi kwa kipindi cha maisha yako yote (WAC 182-527-2734). Jimbo linaweza kurejesha gharama baada ya mauzo ya nyumba, au mali yako ya urithi, isipokuwa:

- Mwenzi wako anaishi katika nyumba hiyo;
- Ndugu yako anaishi katika nyumba hiyo, ni mmiliki mwenza, na anakidhi baadhi ya vigezo.
- Mtoto wako anaishi katika nyumba hiyo, ni kipofu/mlemavu; au
- Mtoto wako anaishi katika nyumba hiyo, ana chini ya miaka 21.

Pata orodha ya huduma zinazopaswa kurejeshwa gharama chini ya umiliki kabla ya kifo katika WAC 182-527-2734.

Kukabidhi Haki na Kutoa Ushirikiano:

Unaelewa kwamba anakabidhi malipo ya wahusika wengine ya huduma ya kitiba kwa Jimbo la Washington unapopokea kinga ya bima ya Washington Apple Health. Hii inamaanisha kwamba Jimbo la Washington litaitoa bima nyingine yoyote ya afya ambayo inawajibika kisheria kuinga gharama zako zozote za kitiba (hii inaweza kuwa bima ya afya ya mwenzi wa zamani au mzazi ambaye huishi naye tena). Mwenye bima hiyo anaweza kupokea taarifa kuhusu gharama zako za kitiba ambazo zinalipwa kupitia bima yake. Ikiwa unahofia hii inaweza kuleta madhara kwako au kwa watoto wako, unaweza kutuomba tusifanye malipo ya wahusika wengine kwa huduma ya kitiba.

Ufichuzi wa 'Annuity':

Ikiwa wewe au mwenzi wako mnalipwa gawio la 'annuity' na mmekubali mafao ya Matibabu ya Muda Mrefu ya Washington Apple Health (Medicaid), mnapaswa kuitaja Jimbo la Washington kama mnufaika mwingine wa 'annuity' hiyo.

Haki za Usikilizaji wa Shauri la Kiutawala:

Usipokubaliana na uamuzi tulioufanya kuhusiana na bima yako ya afya au huduma za matibabu ya muda mrefu, una haki ya kukata rufani ya uamuzi huo kupitia mchakato wa usikilizaji wa mashauri ya kiutawala. Unaweza pia kumwomba msimamizi au mwanashauri kufanya mapitio ya uamuzi au hatua inayopingwa bila kuathiri haki zako za kusikilizwa shauri lako la kiutawala.

Naelewa taarifa nayotoa ili kuomba au kufufua usaidizi husika itafanyiwa uthibitisho na maafisa wa serikali kuu na wa jimbo ili kubaini kama ni ya kweli. Naidhinisha Mamlaka ya Huduma ya Afya ya Jimbo la Washington (HCA) na Idara ya Huduma za Afya na Jamii (DSHS) kufanya uthibitisho wa mali ili kubaini ustahiki wangu na kuthibitisha usahihi wa taarifa zangu za kifedha. Naelewa HCA na DSHS zinaweza kuchunguza na kuwasiliana na taasisi yoyote ya kifedha kama sehemu ya mchakato wa uthibitisho wa mali. Naelewa idhini hii itakoma baada ya uamuzi wa mwisho wa kukataa maombi yangu, ustahiki wangu wa mafao ukikoma, na nikibatilisha idhini hii wakati wowote kwa kuipa HCA au DSHS notisi ya maandishi. Nikibatilisha au nikikataa kutoa idhini, naelewa kwamba sitakuwa na ustahiki wa programu ya Medicaid kwa Wazee, Vipofu au Walemavu (inayohusiana na SSI) ya Washington Apple Health.

Ubatilishaji au ukataaji wa kuidhinisha uthibitisho wa mali hauathiri ustahiki wa Usaidizi Maalum kwa Wazee (TSOA).

Idara inatoa huduma za uandikishaji wa wapiga kura, ikiwemo uandikishaji wapiga kura kiotomatiki.

Kuomba kujiandikisha au kukataa kujiandikisha kupiga kura haitaathiri huduma au kiasi cha mafao ambacho unaweza kukipokea kutoka shirika hili. Ukihitaji msaada kujaza fomu ya uandikishaji wa wapiga kura, tutakusaidia. Uamuzi wa kutafuta au kukubali msaada ni wako. Unaweza kujaza fomu ya usajili wa mpiga kura ukiwa faragha. Ikiwa unaamini kuna mtu ameingilia haki yako ya kujisajili au kukataa kujisajili kupiga kura, haki yako ya faragha katika kuamua kujisajili au katika kuomba kujisajili kupiga kura, au haki yako ya kuchagua chama chako mwenyewe cha siasa au upendeleo mwingine wa kisiasa, unaweza kuandikisha malalamiko katika Washington State Election Division, PO Box 40229, Olympia, WA 98504, email elections@sos.wa.gov, au piga simu 1-800-448-4881.

Je, unataka kujisajili ili kupiga kura au kusasisha usajili wako wa mpiga kura? Ndio Hapana

Usipotiki kisansuu chochote, tutachukulia kwamba umeamua kutojiandikisha kupiga kura kwa sasa, isipokuwa kama una ustahiki, na hujakataa, uandikishaji wapiga kura kiotomatiki.

Isipokuwa kama umetiki “Hapana” hapo juu, unaweza kuwa na ustahiki wa uandikishaji wapiga kura kiotomatiki. Una ustahiki wa uandikishaji wapiga kura kiotomatiki ikiwa utakuwa na angalau miaka 18 katika uchaguzi ujao, ni raia wa Marekani, na DSHS ina jina lako, anwani ya makazi na ya posta, tarehe ya kuzaliwa, uthibitisho wa taarifa ya uraia, na saina yako inayothibitisha ukweli wa taarifa iliyotolewa kwenye maombi haya.

Je, unataka kuandikishwa kiotomatiki kupiga kura? Ndio Hapana

Ikiwa umetiki kisansuku cha “Ndio”, na hujatiki kisansuku kingine chochote na unakidhi matakwa ya ustahiki wa uandikishaji mpiga kura kiotomatiki, DSHS itatuma taarifa zako kwa Ofisi ya Waziri wa Mambo ya Nje na utaandikishwa kiotomatiki kupiga kura.

Ukitaka kutoa maoni au kujumuisha taarifa zaidi, ambatisha karatasi ya ziada.

Nimesoma na kuelewa taarifa iliyo kwenye maombi haya. Nathibitisha, chini ya adhabu ya kusema uongo kwa mujibu wa sheria za Jimbo la Washington, kwamba taarifa niliyotoa katika maombi haya, ikiwemo taarifa kuhusiana na uraia na hali ya uhamiaji ya wanakaya wanaoomba mafao, ni ya kweli, ni sahihi, na kamili kadri ya uelewa wangu.

Saini ya mteja

Nambari ya simu

Tarehe

Saini ya mwenzi

Nambari ya simu

Tarehe

Saini ya mzazi wa mteja ambaye ni mtoto kisheria

Nambari ya simu

Tarehe

Saini ya mwakilishi au aliyeidhinishwa au msaidizi

Nambari ya simu

Tarehe